OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI MVUHA

Halmashauri ya (W) Morogoro,
Phone: 0789895232, 0785725079

Mkuu Wa Shule,
Shule ya Sekondari Mvuha,
P.O.BOX 1644,
Morogoro.
18/12/2020.

E-mail: davidpnduye@gmail.com

KWA MZAZI WA MWANAFUNZI .....

SHULE YA MSINGI .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MVUHA

WILAYA YA MOROGORO MWAKA 2021

1. 0 Nina furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga shule ya sekondari Mvuha kidato cha kwanza mwaka 2021. Muhula wa kwanza masomo yataanza tarehe 04/01/2021 hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 04/01/2021 bila kukosa.

2. 0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule

- Sare ni shati nyeupe mikono mifupi, T-shirt rangi ya bluu inapatikana shuleni, sweta rangi ya kijani.
- Wasichana watavaa sketi ndefu za rangi ya kijani zinazowafika kwenye vifundo viwili vya miguu
- Wavulana watavaa suruali za rangi ya kijani kibichi zisizobana na zenye malinda. (model haziruhusiwi)
- Kila mwanafunzi awe na nembo kwenye sare ya shule (inapatikana shuleni)
- Viatu vyeusi vinavyopakwa dawa. Siyo raba wala bajaji.
- Soksi kwa wasichana ni rangi nyeupe na kwa wavulana ni rangi nyeusi.
- Wanafunzi wa kiislamu wasichana watavaa kanzu fupi inayovuka makalio na pana.

2.2 Vifaa vya usafi kilimo: Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo

i. Mifagio ya ndani na nje
ii. Ndoo ndogo ya lita 10,
iii. Jembe
iv. Kwanja

3. 0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

3.1 **Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978.** Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopangiwa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako.

Scanned by CamScanner

f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki katika Disco, Night clubs, vigodoro, Muziki usiku au mchana.
j. Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele
k. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutoa meza au kiti nje ya darasa bila ruhusa ya mwlimu.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
8. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza harakati zozote zinazoashiria uvunjifu wa amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi.

4. 0 Mambo mengine muhimu

a. Fomu ya uthibitisho wa Afya itakayojazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali (medical examination form). Pamoja na fomu ya kiapo cha mzazi na mwanafunzi. Fomu hizi zitakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara baada ya mwanafunzi kuripoti shuleni.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MVUHA

.....

DAVID PETER NDUYE
Mkuu wa Shule

THE HEADMASTER
MVUHA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 1644
MOROGORO

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Ijazwe na Mzazi au Mlezi)

Mimi ..... Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi ..... kutoka shule ya Msingi ..... Ninaahidi kwamba nitamtunza kijana wangu ambaye ni ..... Kwa kipindi chote cha masomo yake atakapokuwa shuleni na kuhakikisha kwamba mwanangu atatii na kuziheshimu sheria zote zilizowekwa shuleni vilevile nitamtekelezea mahitaji yake yote muhimu ili aweze kuendelea na masomo yake.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi .....

Jina Mzazi/Mlezi .....

SEHEMU B: (Ijazwe na Mwanafunzi)

Mimi ..... Dini yangu ni ..... Shule ninayotoka ..... jina la mzazi/mlezi wa kiume ni ..... Jina la mzazi/mlezi wa kike ..... Nikiwa kama mwanafunzi wa Mvuha Sekondari ninaahidi kuwa nitazitii na kuziheshimu sheria zote za shule.

Sahihi ya Mwanafunzi .....

Jina Mwanafunzi .....

Fomu hii irudishwe pindi mwanafunzi anaporipoti shuleni.

Scanned by CamScanner

MEDICAL EXAMINATION FORM

THE HEADMASTER,
MVUHA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 1644,
MOROGORO.

TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER IN RESPECT
TO ALL FORM I ENTRANTS

PUPIL'S FULL NAME .....

AGE ..... (YEARS)
BLOOD COUNT (RED AND WHITE) .....
STOOL EXAMINATION .....
URINE ANALYSIS .....
SYPHILLIS TEST .....
T.B. TEST .....
EARS .....
CHEST .....
ABDOMEN .....
SPLEEN .....

ADDITIONAL INFORMATION

E.g. Physical defects or impairments, infection chromic of family diseases Etc.
.....
.....
.....
.....
.....

I certify that above is fit/unfit for admission into a day/boarding school.

Signature: ..... Designation: .....
Station: .....
Date: .....

Note: Medical officer, at the time of examination please treat the individual for any illness you note/employee. This complete form should be sent to the Head of the school.
No pupil or person may be enrolled without certification of physical fitness.

Scanned by CamScanner